BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

POMADE
YA MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

'JOB HUNDRED'

KATIKA ENZI za Ukoloni, kulitokea mechi moja baina ya timu mbili zenye wachezaji wa Kiafrika. Mchezo huo wa soka ulichezeshwa na Mzungu. Fowadi hatari wa timu moja akawakata chenga mabeki wawili na kufunga. Mmoja wa mabeki hao alianguka kwa jinsi aliyopigwa chenga.

BILA shaka hilo lilikuwa bao maridadi lilofungwa kiufundi kutokana na vile fowadi alivyowapanga beki mmoja baada ya mwingine na vutio zaidi lilikuwa la jinsi beki mmoja alivyokubali chenga na kwenda moja kwa moja chini na kulala chali!

Mpiga kipenga Mzungu hakusita wala kubabaika na akaonyesha mpira huo ukaanze katikati ya uwanja, aklwa na maana kwamba amelikubali kuwa hilo lilikuwa bao ama goli halali.

Beki huyo alibishana na kila mmoja wakiwemo wachezaji wenzake. Alishikilia msemo huo huo kwamba "hili sikubali sio goli, humuoni yule **JOB HUNDRED!**. *Ikawa pata-shika mpaka maafisa wa timu yake wakaingia kiwanjani.*

Hapo ndipo akawaambia: "Mimi nasema Kizungu nyinyi hamuelewi mbona? Maana ya 'Job' ni kazi na maana ya 'Hundred' ni Mia. Je, nyinyi mkichanganya hamuoni nasema yule mchezaji 'Kazimia'?" Jumaa wakabaki wakicheka!

TAIB MANSWAB

ASEMA MHARIRI

KWA UCHACHE kabisa, leo napendelea nirudie yale ambayo nimewahi kuyazungumza wiki mbili zilizopita kuhusu ongezeko la nauli ya mabasi yanayokwenda kisiwani Lamu. Sina chuki wala vita na wenye mabasi, lakini kwa hali ilivyo, imenilazimu niseme!

ONGEZEKO la petroli pamoja na vifaa vya spea hutokea kila wakati lakini wenye mabasi ya kwenda sehemu nyingine hawaengezi nauli kila mara. Lakini wenzetu wenye mabasi ya Lamu, kila petroli ikipanda nao nauli juu!

TUJIULIZENI sisi wasafiri wa kutoka Mombasa hadi Lamu na Lamu hadi Mombasa: Je, ni mara ngapi nauli ya kutoka Nairobi hadi Mombasa na kutoka Mombasa hadi Nairobi imeongezwa na kwa kiwango gani? Tujiulize tena: wapi mbali- Nairobi/Mombasa ama Mombasa/Kikoni?

LAMU

BASI ikiwa nauli ya Nairobi hadi Mombasa imebakia kuwa 100/- kwa kipindi kirefu na baada ya kuongezeka kwa bei yapetroli, basi kwa nini wasafiri wa Lamu wameongezewa nauli kwa kiasi kikubwa ambacho hakistahiki? Je, maongezo hayo ni ya haki ama ni kwa ajili wanaona kuwa lazima watu watasafiri?

SERKALI inastahili kutumia haki kuhusu ongezeko lolote la nauli. Wenye mabasi ya Lamu wasiumizwe na bali wasafiri pia wasipatiwe taklifu. Kwa nini mzigo mkubwa umewaelemea wasafiri pekee hali wenye mabasi wanazidi kunufaika kwa ongezeko kubwa la 20%?- **ABDULRAHMAN SHERIFF**

• BW. MAHENDO

Cheo Cha Soka

SHRIRIKISHO la Soka (kff) Pwani limetangazwa kusimamishwa uongozini kwa Katibu, Bw. Hamisi A. Mahendo (kushoto) na madaraka yake yamechukuliwa na Bw. Ali Kibwana (hatuna picha yake). Nafasi ya Naibu Katibu imechukuliwa na Bw. Zebedee Muchuka (kulia) aliye pia Katibu Ratiba wa tawi hilo. (Na Abdulrahman Sheriff).

• BW. MUCHUKA

Anayepinga Ya Mtume M. Huwa Ashaukuwa 'Murtad'

na ISIHAKA MTAMBUA

C. MWENYE kuyakanusha yale aliyokuja nayo mjumbe wa mwisho wa Mweny-ezi-Mungu, Mtume wetu Mohammad (S.A.W.) wanaosema hili linafaa kwa kupenda kwao, na hili halifai. Yule yeyote anayepinga alilokuja nalo Mjumbe huyu wa Menye-ezi-Mungu, amezipinga amri za Mola wake, na ameshakua "Murtad".

Kwa haraka anahitajika kusilimu upya, na kupiga shahada maana huwa ameshaingia katika kundi la ukafiri na lau atakufa saa hiyo hiyo atakufa akiwa ni kafiri.

JIHAD

Mwenye-ezi-Mungu (S.H.W.) ametufahamisha katika Qur aan "Enyi mulioamini mwenye kuregea nyuma na kuiacha dini ya Mwenye-ezi-Mungu, Mwenye-ezi-Mungu atawaleta watu wengine awapendao na wampendae yeye, tena waliolaini katika kuamini sio wagumu. Walio na huruma na sikitiko kwa waumini na wakali kwa wale wasiokuwa katika dini. Wale wanaopigana 'Jihad katika njia ya Mola wao, wala hawaogopi lawama la mtu mtu yeyote".

Hizo ni katika fadhla zake Mwenye-ezi-Mungu humpa amtakaye katika waja wake na haswa yule anayestahili kupewa. Mwenye-ezi-Mungu ni Mkunjufu anatoa bila ya kuchelea, ama kuogopa kitu chochote. Tena ni Mjuzi. Maneno haya yaliyotangulia yalipokuwa yanasomewa Makureshi, walikuwa wakiona jambo la ajabu, wakiulizana itakuwaje, ama itawezekanaje waja Mwenye-ezi-Mungu kuja kuiacha dini hii.

Lakini baada ya kufa kwa

ITIKADI

Mtume, wale wale waliokuwa wakisomewa nayo (Islam). Walibakia watu wa Madina, Makka na Twaif peke yao ndio walijidhatiti katika Itikadi zao na wengine wote wakaritadi.

Wengine wakatoka dini kabisa na wengine wakachagua "Kuswali" peke yake na kukataa kutekeleza nguzo ya "Zaka". Kutokea kwa kitendo kama hicho ni thibitisho kwetu kwamba "Qur'aan" ni kitabu kitakatifu chenye miujiza, kinazungumzia mambo ambayo hayajaja, na huja yakatokea baadaye.

Wale wale waliokuwa wakimfuata Mtume kwa utiifu alipokufa, Wakartadi na kulazimika Maswahaba badala yakupigana Jihad na wasiokuwa waumini, wakalazimika kupigana vita na wale waliotoka katika dini, na kuwarudisha.

KILICHOUTEKA ULIMWENGU WA KIISLAMU NA KUUZA-MISHA: Tangu mwanzo wa utawala wa Kiislamu mpaka mwisho wake, hakuna sehemu itakayobakia katika ulimwengu huu, ila utaona kila mahali yuko, ama anapatikana mtu mmoja ambaye amertadi.

Kitendo hiki cha kurtadi ni chenye kuwapiganisha vita jamii nyingi ulimweguni, na kinapatikana majumbani, vyuo vikuu, makollejini, shule za msingi, na mashirika mengi humu ulimwenguni ya Kiislamu. Hakuna jamii inayoweza kujigamba imeepukana na kitendo kama hiki, ila wale waliolindwa na Mwenye-ezi-Mungu.

Hakuna jamii inayoweza kudai imeendelea kidini, ila miongoni mwao wapo, ama yupo mmoja anayeitakidi dini hii ya Mwenye-ezi-Mungu haina faida, ama si yenye manufaa yeyote kwao. Ama kuna wanaopendelea kurtadi binafsi, ama kukitukuza kitendo chenyewe kwa kujishirikisha na baadhi ya wale waliozama katika mambo yanayomtoa mtu katika dini.

Vile vile watu kama hao ndio huwa wanambele wakuyapinga mipango yoyote ya kidini, huwa hawana haja yeyote na mambo ya kidini, isipokuwa wanapendelea anasa na mambo ya kilimwengu tu. (ITAENDELEA....

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

CROSSWORD No. 188

KWENDA KULIA: 1. Wakati wa mvua kubwa. 5. Sumbua, kera. 7. Chombo cha mawasiliano. 9. Umoja wa mataifa. 10. Sehe moja ya mnyama. 11. Mnyama mjanja. 13. Piga mafungu. 14. Isipokuwa. 16. Kataa. 19. Mnyama wa kufugwa. 20. Coastweek.

KWENDA CHINI: 1. Maji yenye harufu nzuri. 2. Mji katika Tanzania. 3. Ama. 4. Inuka. 6. Katika duka. 8. Choma, tia sindano. 10. Mta hamadiliki. 12. Nguvu hasa za mungu. 15. Siku tuliyonayo. 16. Ufupi wa kitambulisho. 17. Yake kwa wingi. 18. Kama 20 kwenda kulia.

Majibu ya shindano la Fumbo la Kujaza Maneno No. 187. Kwenda Kulia: 1. FARUCCI. 6. DO. 7. MISHAHARA. 8. IS. 10. TAO. 12. IE. 13. WA. 14. LA. 15. AMUENI. 19. ENEZA. 20. KUA. 21. KENYA. *KWENDA CHINI:* 1. FUMBO. 2. UDHI. 3. COASTWEEK. 4. IWAPO. 5. CHANGAMKA. 9. KEMEA. 11. AANZE. 12. JA. 16. UN. 17. IAN.

Washindi watatumiwa zawadi zao na Coastweek.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 187.

1. Shomari Nyawa, Sanduku La Posta Mazeras S. School, P.O. Mazeras Mombasa. 2. Chiuzo K. Swaleh, Sanduku La Posta 87081, Mombasa. 3. Bakari Juma Sanduku La Posta 90581, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata viatu na 'Bint El Sudan - Gift Pack'. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili ipelekwe kwa Mhariri COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe June 20 1984 saa mbili asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.

JINA..

SANDUKU LA POSTA...................................

MWILI wa Marehemu Bw. Asaph Mureria, aliyekuwa Mkuu wa Afisi ya Gazeti la "The Standard" ulipokuwa ukisafirishwa kutoka uwanja wa Ndege wa Moi, Mombasa kuelekea nyumbani kwake Nyeri. PICHA: CAESAR MAHDANGANHA

HARUSI ya kufana ilifanyika katika Kanisa la Methodist, Pangani. Bwana Harusi alikuwa Ambrose Gwirah anayefanya kazi katika hoteli ya Kitalii ya Jadini Beach Hotel hali Bibi Harusi Sarah anafanya kazi katika Mahakama ya Mombasa.